



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA



Tarehe:13/05/2024

YAH: TANGAZO LA ULIPAJI WA KODI YA PANGO LA ARDHI.

Mkurugenzi Mtendaji anawatangazia Wananchi wote wanaomiliki viwanja ndani ya Halmashauri kulipa kodi ya pango la ardhi, Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi sura 113 kifungu cha 33(1) inayowataka wamiliki wa viwanja kulipa kodi ya pango la ardhi kila mwaka. Pia Kifungu cha 44(1) cha Sheria hiyo kinawataka kila mwananchi anayemiliki kiwanja anatimiza wajibu huo kulipa kodi ya ardhi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha Sheria ya Ardhi (sura ya 113) wamiliki ambao hawajalipa kodi ya pango la ardhi watafikishwa mahakama na kwa mujibu wa Kifungu cha 45 ya Sheria ya Ardhi (sura ya 113) taratibu za kisheria za ubatilisho wa miliki zao zitafanyika.

Kila mmiliki wa kiwanja anatakiwa kutimiza wajibu wake ili kuepuka usumbufu.

Limetolewa na;


Haji M. Mnasi, PhD
MKURUGENZI

MKURUGENZI MTENDAJI (W.)
SIHA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, 5 BR Sanya Juu - Elerai, S.L.P. 129, 25482 Siha - Kilimanjaro

Simu: 0272-970677 Nukushi: 027-2970678

Barua pepe: ded@sihadc.go.tz Tovuti: www.sihadc.go.tz